

Maelekezo ya usanifu

Uniti ya 2 ya CID

Fremu ya Picha

Vifaa:

- Fremu ya picha ya familia (1 kwa kila mwanafunzi)
- Herufi za mapovu "CID" (1 kwa kila mwanafunzi)
- Lenzi ya kuongeza ukubwa ya mapovu (1 kwa mwanafunzi)
- Kurunzi/tochi ya mapovu (1 kwa kila mwanafunzi)
- Kipande kimoja cha utepe uliosokotwa (1 kwa kila mwanafunzi)
- Gundi

Badala ya mapovu, unaweza kutumia karatasi nzito au karatasi ya rangi.

Maagizo:

1. Mpe kila mtoto vipande vyake.
2. Fanya watoto waweke vipande kwenye fremu ya picha wakitumia gundi.
3. Weka utepe uliosokotwa upande wa juu kwa mpindo ili kutundika.
4. Waelezee watoto kwamba wanapofika nyumbani, wanaweza kupaka rangi katika picha au kuweka picha upande wa nyuma. Wafundishe jinsi ya kuiweka vizuri kwa kutumia gundi.

Mapambo ya CID

Vifaa:

- Herufi kubwa "CID" (1 kwa kila mwanafunzi)
- Miraba ya karatasi ya tishu ya kila rangi (50 kwa mwanafunzi)
(Karatasi ya tishu ni karatasi ya rangi ambayo ni nyembamba sana / karatasi ya Kichina.)
- Gundi
- Penseli



Maagizo:

1. Patia kila mtoto herufi kubwa za "CID", na miraba 50 ya tishu / karatasi ya Kichina.
2. Ukitumia penseli, funga karatasi ya tishu imara juu ya kifutio cha penseli.
3. Funika sehemu ya kifutio cha penseli kwa kutumia gundi.
4. Weka karatasi ya tishu kwenye herufi za "CID" kwa gundi.
5. Endelea mpaka herufi "CID" ziwe zimefunikwa na karatasi ya mapambo ya tishu.

Beji ya Nyota

Vifaa:

- Nyota ya povu (1 kwa kila mwanafunzi)
- Nyota ya karatasi (1 kwa mwanafunzi)
- Sekuini au shanga za mapambo (10 kwa mwanafunzi)
- Pini za nguo (1 kwa kila mwanafunzi)
- Gundi



Badala ya mapovu, unaweza kutumia karatasi nzito au karatasi ya rangi.

Nini cha kufanya:

1. Patia kila mtoto nyota ya povu, nyota ya karatasi na sekuini.
2. Fanya watoto waweke nyota ya karatasi kwenye nyota ya povu wakitumia gundi.
3. Fanya watoto waweke sekuini kwenye pointi za nyota zote mbili wakitumia gundi.
4. Mwalimu au msaidizi awasaidie watoto kuweka nembo ya nyota kwenye mashati yao kwa kutumia pini ya nguo.